**KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA-KKKT**

**EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA-ELCT**

**PARE DIOCESE**
**Kirangare Lutheran Parish**

**SUNDAY SERVICE SEPETEMBER 17, 2023 at Mpare Preaching Point**

**15TH SUNDAY AFRET THE HOLY TRINITY**

**Leader:** Wapendwa katika Bwana: Tuanze ibada ya siku hii ya Bwana ya 15 baada ya Utatu Mtakatifu, katika Jina la Baba, na la Mwana , na la Roho Mtakatifu. Amen.

**Congr: Amen.**

1st Reading: Psalm 37:23-26

2. Choir

3. Hymn number 434 (TMW)

4. Liturgy Page 250

**Leader:** Ee Bwana, Muumba, Mkombozi, na Mfariji wetu, tunapokusanyika kukuabudu kayika roho na kweli, twakuomba kwa unyenyekevu utufungue mioyo yetu iweze kupokea mahubiri ya Neno lako, ili tuweze kutubu dhambi zetu, kuamini katika Yesu Kristo kama Mwokozi wetu pekee, na tupate kukua katika neema na utakatifu. Utusikie kwa ajili yake. Amen

**Congr: Amen.**

Leader: Bwana Mungu wetu yupo hapa, yu pamoja nasi. Tumsujudie tumche; tumsikie jinsi anavyotufundisha katika Neno lake: Mpende Bwana Mungu wako kwa mooyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zakozote na kwa nguvu zako zote; na Mpende jirani yako kama nafsi yako.

Leader: Msaada wetu ni katika Jinala Bwana.

**Congr: Aliyeziumba mbingu na nchi.**

**UNGAMO LA DHAMBI (CONFESION OF SINS)**

Leader: Wapendwa katika Bwana: Tumekusanyika mbele za uso wa Mungu kumtukuza kwa ajili ya neema yake na uaminifu wake; kusikia Neno lake takatifu, na kuomba ahuishe roho na miili yetu. Kwakuwa Mungu ni Mtakatifu, na sisi tu wenye dhambi, hivyo basi na tumwungamie Mungu dhambi zetu katika roho ya toba na imani, tukimwomba msamaha wa dhambi:

**Leader + Congr:**

**Mungu Mwenyezi, Baba wa rehema, mimi niliye maskini na dhaifu na kuzaliwa katika hali ya dhambi, naungama mbele zako dhambi zangu zote, nilizozifanya kwa kuwaza, kwa kunena, na kwa kutenda. Nimekukasirisha mara kwa mara. Nikastahili adhabu yako hapa duniani na hata milele. Lakini nazijutia dhambi zangu na kutubu kweli. Nakusihi kwa rehema yako iliyo kuu. Unihurumie na kuniokoa mimi niliye maskini na mwenye dhambi. Eee Bwana, unisamehe dhambi zangu zote, unipe nguvu za Roho Mtakatifu wako, nishike mwenendo mpya. Amen**

**ONDOLEO LA DHAMBI (Absoulution)**

Leader: Mungu mwenyezi na mwenye rehema kwa neema alimtoa Mwana wake wa pekee kufa msalabani. Kwa ajili ya Kristo Mungu ametusamehe dhambi zetu zote. Amen.

**Congr: Amen**

**ANTIPHONE AND PSALM ( pp 290-291)**

Leader : Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu,

**Congr: Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.**

Leader: Eee Mungu wangu, Mfalme, nitakutukuza,

**Congr: Mitalihimidi Jina lako milele na milele.**

Leader: Kila siku nitakuhimidi,

**Congr: Nitalisifu Jina lakomilele na milele.**

Leader: Bwana ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana,

**Congr: Walaa ukuu wake hautambulikani.**

Leader: Ee BWANA, kazi zako zote zitakushukuru,

**Congr: Na wacha Mungu wako watakuhimidi.**

Leader: Ufalme wako ni ufalme wa zamani zote,

**Congr: Na mamlaka yako ni ya vizazi vyote.**

Leader: Atukuze Baba na Mwana na Roho Mtakatifu,

Congr: **Kama ilivyokuwa mwanzo, naiwe sasa na siku zote na hata milele na milele, Amen.**

**KYRIE ( pg. 254)**

Leader: Tumwombe Bwana katika amani.

**Congr: Bwana uturehemu.**

Leader: Ee Bwana, tunakuomba amani ya ulimwengu wote, na umoja wa Kanisa la Mungu.

**Congr: Bwana uturehemu**

Leader:Ee Bwana, tunawaombea wote wanaoingia nyumbani mwako, wanaokuabudu na kukusifu.

**Congr:Bwana uturehemu**

Leader: Ee Mungu, utusaidie, utuokoe, utuhurumie na kutuhufadhi kwa neema yako.

**Congr: Amen.**

**GLORIA IN EXCELSIS (UTUKUFU KWA MUNGU)**

Leader: Utukufu ni wa Mungu juu mbinguni.

**Congr: Amani duniani kwa watu aliowridhia**

**Leader +Congr: Mungu atukuzwe pekee, shukrani zitolewe,sababu ya rehema kuu aliyotutendea. Munguatupenda sana, sababu hii ametupa, kutengemana vema.**

**SALAMU (SALUTATIO)**

Leader:Bwana akae nanyi

**Congr: Akae na roho yako.**

**COLLECT**

**Leader:** 1Peter 5:7 "Mtwikeni yeye fadhaa zetu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu".

Leader (Praying): Ee Bwanaa, pasipo wewe hatuwezi kuushinda udhaifu wetu wa kibinadamu; utusaidie, ullilinde Kanisa lako kwa neema yako daima, utusaidie, tusihangaikie mambo ya dunia, bali tuutafute ufalme wako; kwa yesu Kristo, Mwana wako na Bwana wetu, Amen.

**Congr: Amen**

2nd Reading: Acts 10: 1-8

**IMANI YA MITUME (APOSTOLIC CREED)**

Leader: Tukiri imani yetu ya Kikristo inayotuunganisha sisi na Wakristo wote ulimwenguni.

Congr: (Turn pg No. 257 for Apostolic Creed)

Choir then Announcements

Joint Hymn No. 196 Upendo wa Mungu wetu ( The love of our God)

Baptism ( Hymn No. 167) then pg 363

Chorus for Praise before Sermon (Choir Leads)

Sermon by Pastor Clark Olson-Smith (Matthew 14:28-36)

Choir while congregation giving Offerings for Parish Mission work and Stewardship

Hymn No. 189 **THE LORD'S SUPPER (pp. 270-274)**

Hymn No. 13 ( 1st Stanza) KUOMBEA MATOLEO NA MAOMBEZI (OFFERTORIUM ET INTERCESSIO) P. 259-261

LORD'S PRAYER PG. 265

**Pg. 265: UTUME ( MISSIO)**

**Leader: Bwana akae nanyi**

**Congr:Akae na roho yako**

**Leader: Tumhimidi Bwana**

**Congr:Tumshukuru Mungu**

Leader:

Bwana akubarikie. Na kukulinda,

Bwana akuangazie nuru za uso wake na kukufadhili,

Bwana akuinulie uso wake na kukupa amani.

Katika jina la Baba, na la + Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amen

Congr: Amen, Amen, Aaaamen. Matendo yangu yoyote uyatengeneze Yesu , uniongoze popote. Nitakapokuwa leo. Aaaamen.

Hymn for Leaving the Sanctuary (Hymn No. 195 Mungu awe Nanyi Daima)